**Noa Bongo –Jenga Maisha Yako !**

**Utandawazi : Utalii Senegal**

**O-Töne : Mountanga Amadou Sar**
**Text : Sandrine Balanchard**
**Redaktion : Yann Durand**
**Übersatzung : Anne Thomas**

---

**Wie immer 3 Stimmen ( Sauti 3 )+ Voice Over für O-Ton……**
**- junger Sprecher 1 …………  Msimulizi wa kiume 1**
- **junge Sprescherin 1…….Msimulizi wa kike 1**
- **Sprescher(in ) 2……Msimulizi wa kike 2**
- **als off Stimme für die Reportage**

---

**Voice Over für O-Ton : Wanawake 2,Wanaume 3**

- **1 rzs .Touristin  ………..Mtalii wa kike 1**
- **1 Senegal Minsterin…….Waziri wa kike 1**
- **2 Senegal Verkäufer……Wauza maduka wawili**
- **1 frz Tourist ………… …Mtalii wa kiume**

---

**Vorspann LbE………………………….Kiashirio cha Kipindi**

**SEHEMU YA KWANZA – REPORTAGE  : REPOTI**

**Msimulizi wa kike 1 :** Habari gani ! Natumai nyote hamjambo !

**Msimulizi wa kiume 1 :( enthusiastically ….kwa hamasa)**
Leo katika mfululizo wa vipindi vyetu vya utandawazi tutakwenda katika mapumziko ……..tunachukuwa likizo !

**Msimulizi wa kike 1 :**………tutazungumzia utalii.

**Msimulizi wa kiume 1 :**

**1 . Atmo Meer Möven unterlegen**

**Msimulizi wa kiume 1 :** Na tunaelekea Senegal kituo muhimu cha watalii Afrika magharibi.

**Msimulizi wa kike 1 :** …nchi ambayo inazidi kuchukuwa hatua kila uchao kuendeleza ulimwengu wa kuvutia wa shughuli za utalii.

**Msimulizi wa kiume 1 + Msimulizi wa kike 1**

Kwa hiyo fungeni mikanda yenu tayari kwa safari !

**………………………….Manuscript ………………………..**

**1. Atmo hoch dann unterlegen…………………**

**Msimulizi wa kike 1 :** Ikiwa inachukuwa masaa matano kwa safari ya ndege kutoka takriban mij mikuu mingi ya Ulaya Senegal ni mojawapo ya kituo cha fukwe za kitalii za nchi za joto kilioko karibu sana. Asilimia 70 ya watalii nchini Senegal ni wazungu na wengi wao ni Wafaransa.Hupendelea kufanya safari fupi za wiki moja.

**2.O-Ton Mtalii wa kike :**

Tuko watatu …..mrafiki watatu….tumeamua kuichaguwa Senegal kwa sababu hatuijuwi Afrika.Tulikuwa tunataka kuvumbuwa mambo pamoja na kuota jua.

**3.Atmo Schiff hoch dann unterlegen …………**

**Msimulizi wa kike 2 :** Zaidi ya nusu ya watalii wanaokwenda Senegal wanakwenda huko ajili ya fukwe zake.Katika bahari ya Atlantiki nchi hiyo ina kilomita 700 ya safu ya mwambao na kilomita

400 za fukwe. Senegal pia ina maeneo kadhaa yanayotambuliwa kuwa ya urithi wa dunia na UNESCO.

**Msimulizi wa kiume 1 :** Kwani UNESCO ni nini ?

**Msimulizi wa kike 1 :** UNESCO ni shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu,Sayansi na Utamaduni.Shirika hili linahifadhi maeneo ya urithi wa kitamaduni na asili ambayo yanahesabiwa kuwa na thamani kubwa ya kupigiwa mfano kwa ubinaadamu.Kuna takriban ofisi 15 za UNESCO katika eneo la kusini mwa Jangwa la Sahara barani Afrika.

**4.Atmo Goree……………………..**

**Msimulizi wa kike 2 :** Naam tuko tena Senegal. Maeneo ya urithi wa dunia ya UNESCO ni pamoja na kisiwa cha Goree ambacho kiko umbali wa kilomita nne kutoka mji mkuu wa Dakar.Hapo kuna makumbusho moja inayoitwa Nyumba ya Watumwa ambayo imehifadhi kumbukumbu ya historia ya mamilioni ya watumwa wa Afrika ambao walisafirishwa kwa nguvu kwa meli kuelekea kwenye ulimwengu wa nje ya bara hilo. Na nje ya makumbusho hiyo kuna wafanyabiashara wanaouza vitu kama vile vinavyouzwa nje ya kila eneo la utalii duniani.

**5.O-Ton Moussa Toristen …………..Mousa Utalii**

Hupendelea watalii kwa sababu huwa wanalipa vizuri zaidi kuliko wananchi wa Senegal.

**Msimulizi wa kike 2 :** Lakini kuna watalii wengine kama vile Michel Pinorini hawapendi kuandamwa na wachuuzi

**6.O-Ton Pinorini**

Fikra yangu juu ya Dakar ni mahala ambapo biashara inajaribu kukua lakini kuna wafanyabishara wengi mno na watu wanaouza kila aina ya upuuzi.Wakati unapoona jinsi vibanda vya biashara vilivyokuwa vingi kimoja baada ya kengine kwa kweli unajiuliza huwa wanauza kiasi

gani kwa siku na iwapo kweli wanaweza kuishi kwa kutegemea biashara hiyo.

**Msimulizi wa kike 2 :** Pape Mbaye ni mfanyabiashara wa vitu vya asili vya thamani katika soko la Kermel mjini Dakar.Anasema kwamba kumezidi kuwa na wateja wachache wa kigeni kila siku inaposonga.

**7.O-Ton Pape Mbaye**

Ni kwa sababu ya mahoteli.Wamiliki wa mahoteli hayo hivi sasa wanawekeza katika maduka ambayo huuza vitu kwa wageni wa mahoteli.

**Msimulizi wa kike 2 :** Aminata Lo Dieng ni waziri wa utalii nchini Senegal ambaye anataraji kwamba wigo wa utalii utatanuka.Angelipenda kuendeleza utalii utakaozingatia utunzaji wa mazingira na pia utalii wa kibiashara.Ili kufanya hivyo serikali sio tu inabidi iboreshe miundo mbinu bali pia iwapatie mafunzo vijana.

**8.O-Ton Waziri Mafunzo…..**

Kumekuwepo na chuo kimoja ambacho kilikuwepo hapa tokea mwaka 1959.Lakini nataka kuanzisha vyuo vingi zaidi na taasisi ya elimu ya juu kwa ajili ya shughuli za hoteli na utalii.Hivi sasa tunanzisha mradi wa kuwapatia fursa vijana ya kujipatia uwezo wa sifa katika biashara.Tunataka kuwa na aina ya watu ambao watakidhi mahitaji mapya.

**Msimulizi wa kike 2 :** Ukichangia faranga bilioni 300 za CFA sarafu inazotumiwa na makoloni ya zamani ya Ufaransa utalii ni chanzo cha mapato cha pili kwa ukubwa kwa Senegal ikitanguliwa na biashara ya uvuvi.Lakini kuna mapugufu yake hapo.Baadhi ya watalii hawana utashi na Senegal au wanakuwa hawakujulishwa vyema.Wengine wanakuwa hawaonyeshi heshima kwa nchi mwenyeji,kwa wananchi au kwa utamaduni wa wenyeji,Utalii wa ngono ni moja ya tatizo kubwa.

**Msimulizi wa kiume 1 :** Utalii wa ngono ???

**Msimulizi wa kike 1 :** Ni wakati wanaume au wanawake kwa kawaida kutoka mataifa ya magharibi wanapokwenda katika nchi ya kimaskini kwa ajili ya kuwa na uhusiano wa kingono na wananchi wenyeji. Kutokana na umaskini wenyeji wanauza miili yao ili wajipatie fedha au zawadi.Mamia kwa maelfu wanauza miili yao kila mwaka wakiwemo watoto.

**Msimulizi wa kiume 1 :** Lakini huo ni ukahaba?

**Msimulizi wa kike 1 :** Utalii wa ngono ni biashara haramu inayoshika nafasi ya tatu baada ya biashara ya madawa ya kulevya na silaha.Kila mwaka inakadiriwa kuwepo kwa watalii milioni 80 duniani kote.Na bisahara hiyo inazidi kupamba moto katika nchi za kimaskini.

**Msimulizi wa kike 2 :** Na ndio maana ni muhimu kuweka sheria kali zaidi kupambana na tatizo hilo.Aminata Lo Dieng analifahamu vizuri suala hilo.

**9.O-Ton Waziri Ngono**

Inabidi tuanzishe hatua za kuviadhibu vitendo fulani na tunatakiwa tuwapatie mafunzo bora zaidi waongozaji watalii. Inabidi tuhakikishe kwamba utalii haujipatii sifa mbaya miongoni mwa wananchi wetu na hususan miongoni mwa kizazi chetu kichanga.

**Msimulizi wa kike 2 :** Lakini utalii pia ni kuhusu safari,kuvumbuwa mambo,kukutana na watu …kwa ufupi ni kuhusu kufurahia kuwa na mawasiliano mapya na mahala pengine na watu wengine ambao kwa kweli hawako tafauti hivyo na hawako mbali hivyo….

**10.O-Ton Touristin Abreise 1.10………..Mtalii wa kike……**

Hata kama nchi inakuwa inavutia na nzuri inabidi uondoke ili kwamba uweze kurudi tena.

**MWISHO WA SEHEMU YA KWANZA**

**Music hoch dann unterlegen und ausblenden ………………….**

**SEHEMU YA PILI  ERKLÄSTUCK……………**

**Msimulizi wa kiume 1 na Msimulizi wa kike 1 tu**

**Msimulizi wa kiume (etonne)………….:**

Kwa hiyo utalii sio kuhusu mapumziko tu !

**Msimulizi wa kike (amusee) :**

Hapana sio kuhusu mapumziko tu!Utalii ni shughuli nambari moja duniani.Umoja wa Mataifa una hata chombo maalum cha utalii………WTO.

**Msimulizi wa kiume :** Shirika la Utalii Duniani .

**Msimulizi wa kike :** Hasa ! Shirika hilo la Umoja wa Mataifa la Utalii Duniani linasema idadi ya watalii inaongezeka kwa asilimia 4 kwa mwaka. Kwa kuzingatia kiwango hiki kutakuwa na watalii bilioni 1.6 hapo mwaka 2020.

**Msimulizi wa kiume :** Takriban watalii wote ni wa mataifa ya magharibi kwa sababu ni matajiri kuliko watu wengine ?

**Msimulizi wa kike :** Kwa ujumla ndio …na pia kuna likizo za malipo katika nchi nyingi zilizoendelea.Watu huwa wanalipwa mishahara yao hata kama wako katika mapumziko.Wajerumani hupata wiki sita za mapumziko kwa mwaka.

**Msimulizi wa kiume :** Nimelipenda wazo hilo….,……lakini vipi utandawazi unahusika na yote hayo ?

**Msimulizi wa kike :** Naam utandawazi umesaidia wale wenye kuwa na uwezo kusafiri nchi za nje….kwa mfano ushabiki wa safari za ndege pia umesaidia.

**Msimulizi wa kiume :** Lakini fungu la Afrika la utalii wa kimataifa bado ni dhaifu sana..

**Msimulizi wa kike :**Ni kama asilimia 3 hivi na kwa kiasi kikubwa kutokana na uhaba wa miundo mbinu,barabara mbaya na usafiri wa reli.Lakini idadi ya utalii inaongezeka duniani na pia Afrika.

**Msimulizi wa kiume :** Lakini inaongezeka kwa kiasi gani kwa mwaka?

**Msimulizi wa kike :** Kwa milioni 22.Afrika Kusini, Botswana,Namibia,Kenya na Zimbabwe ni mahala ambapo nusu ya watalii wa Afrika hutembelea.Utalii ndani ya bara lenyewe la Afrika bado hakuendelezwa.

**Msimulizi wa kiume :** Kuna pia vilabu vya mapumziko…..

**Msimulizi wa kike :** Utalii wa makundi makubwa sio mashuhuri sana katika nchi zilioko kusini mwa jangwa la Sahara barani Afrika.

**Msimulizi wa kiume :** Inaonekana kinyume kidogo kuona mabwawa ya kuogelea katika maeneo ambapo hakuna maji kabisa ……

**Msimulizi wa kike :**

……..na kuhusiana na utalii wa aina nyengine ….kama vile unaozingatia utunzaji wa mazingira,utalii unaozingatia masuala haki, utalii wa kuwajibika yumkini sio mashuhuri sana lakini mahitaji yake yanaongezeka.

**Msimulizi wa kiume :** Miongoni mwa watu wanaotaka kuchanganya mapumziko yao na heshima kwa ajili ya watu wanaokutana nao wakati wakiwa nchi za nje.

**Msimulizi wa kike :** Ndio sawa kabisa  bwana !

**Outro ……………….Funga Kipindi**

**Msimulizi wa kike 2 :**

Na kufikia hapo ndio tunahitimisha kipindi chetu cha Noa Bongo Jenga Maisha Yako.Asante kwa kusikiliza kipindi hiki juu ya utandawazi na ulimwengu wa utalii.Ni kipindi cha Deutsche Welle kilichotayarishwa na Mountaga Amadou Sarr na Sandrine Blanchard.Ili kujuwa zaidi na iwapo unataka tena kusikiliza kipindi hiki tafadhali nenda kwenye tovuti yetu  :  www.dw-world.de/be
Usikose kujiunga nasi tena mara nyengine.
Kwaheri!